**MAHITAJI MUHIMU YA KUOMBA MKOPO WA ELIMU YA JUU HESLB 2025/2026**

## 1. TAARIFA ZA USAJILI

**Kinachohitajika:**

- Namba ya Mtihani Kidato cha Nne (CSEE) na Kidato cha Sita (ACSEE)
- Namba ya simu ya mwombaji
- Anwani ya barua pepe (Email address)
- Ada ya maombi Tsh. 30,000/= kwa Degree, 20,000/= kwa Diploma

**Kwa nini kinahitajika:**

- Kuhakikisha usajili sahihi wa mwombaji
- Mawasiliano ya moja kwa moja kutoka HESLB
- Ada ni kwa ajili ya kuchakata maombi

**Kinapatikanaje/Wapi:**

- Ada inalipwa kwa kutumia *Control Number* kutoka kwenye mfumo wa HESLB (OLAMS)
- Malipo yanafanyika kwa simu kupitia miamala ya benki au mitandao ya simu

---

## 2. TAARIFA ZA KUZALIWA

**Kinachohitajika:**

- Tarehe ya kuzaliwa
- RITA Verification Code ya cheti cha kuzaliwa (kutoka RITA)

- NIDA (kwa waliotimiza miaka 18+)
- Cheti cha kifo cha mzazi (ikiwa mzazi/wazazi wamefariki)
- Mkoa, Wilaya uliozaliwa
- Picha ya Passport (background ya blue)

**Kwa nini kinahitajika:**

- Kuhakiki umri na uhalali wa mwombaji
- Kwa yatima, cheti cha kifo ni uthibitisho wa hali ya familia

**Kinapatikanaje/Wapi:**

- RITA Verification Code: https://verifi.rita.go.tz au ofisi za RITA
- Cheti cha kifo: Ofisi ya RITA au halmashauri ya wilaya uliyozaliwa
- NIDA: https://nida.go.tz au ofisi za NIDA

**Muda wa Kupata:**

- RITA: 3–7 siku
- NIDA: Wiki 1–3
- Cheti cha kifo: 1–7 siku (kutegemea uthibitisho)

---

**3.TAARIFA ZA MAKAZI YA KUDUMU (NAPA)**

**Kinachohitajika:**

- S.L.P, Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji/Mtaa
- Posti kodi ya mtaa
- Namba ya nyumba
- **NAPA Reference Number**

**Kwa nini kinahitajika:**

- Kudhibitisha makazi ya mwombaji

**Kinapatikanaje/Wapi:**

- Tembelea Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji
- Waombe wakusajili kwenye mfumo wa **NaPA**

- Baada ya kusajiliwa, nenda https://napa.mawasiliano.go.tz kuomba barua ya utambulisho yenye NAPA Reference Number

**Muda wa Kupata:**

- Siku 1–3 endapo uko tayari kusajiliwa

---

**4.TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI**

**Kinachohitajika:**

- Majina kamili, elimu, kazi, simu, S.L.P, posti kodi, NAPA Reference Number
- Ulemavu wa mzazi/mlezi (ikiwa upo): **Uthibitisho unapaswa kuambatishwa kupitia fomu maalum iliyosainiwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) au Mkoa (RMO)** kulingana na mwongozo wa HESLB
- Upo hai au la (ikiwa hayupo, ambatisha cheti cha kifo)
- Taarifa ya TASAF (ikiwa familia inafaidika)
- Majina kamili, elimu, kazi, simu, S.L.P, posti kodi, NAPA Reference Number
- Ulemavu wa mzazi/mlezi (ikiwa upo)
- Upo hai au la (ikiwa hayupo, ambatisha cheti cha kifo)
- Taarifa ya TASAF (ikiwa familia inafaidika)

**Kwa nini kinahitajika:**

- Hutoa picha ya hali ya kifamilia na kijamii kwa ajili ya tathmini ya uhitaji

**Kinapatikanaje/Wapi:**

- Kupitia taarifa za familia
- TASAF: Namba ya usajili hupatikana kupitia Halmashauri au ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji
- Cheti cha kifo: RITA au Halmashauri

**Muda wa Kupata:**

- TASAF: Endapo uko kwenye mpango, upatikanaji wa namba ni haraka
- Vyeti vya vifo: ndani ya siku 3–7

---

**5.TAARIFA ZA ULEMAVU (Ikiwa unahusika)**

**Kinachohitajika:**

- Taarifa kamili kama mwombaji ana ulemavu
- Aina ya ulemavu
- Cheti cha daktari au uthibitisho kutoka taasisi ya afya/serikali

**Kwa nini kinahitajika:**

- HESLB hutoa kipaumbele kwa waombaji wenye ulemavu
- Kuhesabiwa kwenye kundi maalum la waombaji

**Kinapatikanaje/Wapi:**

- Hospitali za serikali au binafsi zenye usajili halali
- Barua ya uthibitisho kutoka kwa Mganga Mkuu wa Wilaya/Mkoa

**Muda wa Kupata:**

- Cheti kinaweza kupatikana ndani ya siku 1 hadi 5

---

**6. TAARIFA ZA ELIMU**

**Kinachohitajika:**

- Je umehitimu kidato cha sita?
- Namba ya mtihani wa Diploma (kama ulisoma Diploma)
- AVN Number (kutoka NACTVET)
- Chuo ulichosoma, mwaka uliomaliza

**Kwa nini kinahitajika:**

- Kuthibitisha uhitimu wa elimu ya awali

**Kinapatikanaje:**

- Kupitia vyeti halisi
- AVN: https://www.nacte.go.tz

---

## 7. TAARIFA ZA MFADHILI (Kama unao)

**Kinachohitajika:**

- Jina, simu, S.L.P, barua rasmi ya ufadhili

**Kwa nini kinahitajika:**

- Husaidia kuthibitisha kama kuna taasisi inayofadhili

**Kinapatikanaje:**

- Barua ya ufadhili kutoka shirika
- Form ya ufadhili (inapatikana kwenye akaunti ya HESLB wakati wa maombi)

**Tahadhari:**

- Mfadhili lazima awe taasisi inayotambulika kisheria

---

## 7.TAARIFA ZA MDHAMINI

**Kinachohitajika:**

- Jina kamili, jinsia, mkoa, wilaya, kata, mtaa, email
- Kitambulisho (NIDA, Leseni, Passport n.k.)
- NAPA Reference Number, picha ya passport size, posti kodi, namba ya nyumba

**Kwa nini kinahitajika:**

- Kuhakikisha kuna mtu anayethibitisha maelezo yako kama mdhamini

**Kinapatikanaje:**

- Kupitia mdhamini mwenyewe

---

## 9. TAARIFA ZA BENKI

**Kinachohitajika:**

- Jina la akaunti
- Namba ya akaunti
- Jina la benki

**Kwa nini  inahitajika:**

- Fedha za mkopo zitatumwa kwenye akaunti ya benki

**Tahadhari:**

- Majina ya akaunti ya benki **lazima** yafanane na ya vyeti

---

### 🔄 TAARIFA ZA WAOMBAO DIPLOMA/CONTINUING STUDENTS

**Kwa Diploma:**

- AVN Number
- Hakikisha kozi ipo kwenye mwongozo wa HESLB
- Taja chuo na kozi ulizoomba

**Kwa Continuing Degree:**

- Hakikisha umefaulu kwenda mwaka unaofuata
- Kusanya matokeo yako ya chuo kwa loan officer wako
- Taja chuo, kozi, registration number, na mwaka uliopo

---

📝 **MUHIMU:**
Hakikisha taarifa zote ni sahihi na zimehakikiwa kabla ya kutuma maombi. Marekebisho kwenye baadhi ya nyaraka kama cheti cha kuzaliwa au taarifa za NIDA yanaweza kuchukua muda mrefu. Andaa mapema kabla dirisha la maombi halijafunguliwa rasmi.

## 🎓 *University Warm-Up Community Announcement*

Wanafunzi wote mnaotarajia **kuomba mkopo wa elimu ya juu (HESLB)** kwa mwaka 2025/2026, tunawakaribisha kwenye **Group la Msaada** linalosimamiwa na **University Warm-Up Community**.

👥 **Kundi hili ni bure kabisa** na limekusanya:
✅ Wanafunzi waliopo vyuoni waliopata mkopo kwa mafanikio
✅ Wanafunzi waliopitia na kuelewa kwa kina mwongozo wa HESLB
✅ Wataalam wa ushauri kutoka kwa jamii yetu

💬 Kupitia group hili, utaweza:

- Kuuliza maswali kuhusu hatua za maombi
- Kujua nyaraka muhimu zinazohitajika
- Kupata msaada wa moja kwa moja kutoka kwa waliopitia hatua hizo
- Kupata updates muhimu bila kupoteza muda

🧠 **Kumbuka:** *Mandalizi mazuri huleta matokeo mazuri!* Usingoje hadi dirisha la maombi lifunguliwe ndipo uanze kushtuka.

🟢 **Jiunge sasa kwenye WhatsApp group kupitia link hii:**
👉 https://chat.whatsapp.com/KbDffsw60688vEAOE1btJj